Njia ya kuepuka imepeanwa na Biblia inasema, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote." **(1 Yohana 1:9)**

Mungu anakupenda, lakini anachukia dhambi yako. Mungu niwa upendo na mwenye rehema – hataki kutuhukumu. Tena Mungu ni mwenye haki, kwa hiyo ni lazima aihukumu dhambi. Kifo chake Yesu kwa ajili ya wenye dhambi kiliwezesha Mungu Mutakatifu kuendelea kuwa Mwenye haki, na wakati huo huo mwenye kuhesabia haki wale wasiomcha Mungu!

Ndani ya Kristo, "Fadhili na kweli zimekutana, Haki na amani zimebusiana." **(Zaburi 85:10)**

Hata igawa tunastahili mshahara wa dhambi, Mungu kwa neema alitupa KARAMA ya wokovu, uzima wa milele!

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." **(Warumi 6:23)**

Bwana Yesu Kristo alilipa mshahara wa dhambi kwa kifo chake na akatununulia karama ya uzima wa milele kwa damu yake mwenyewe. "Kwa damu ya thamani ya Kristo" **(1 Petro 1:19)**

Karama hii kubwa imepeanwa kwa neema kwako, ndio kwako, Mungu asema, "Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka." **(Warumi 10:13)**, kila yamaanisha YEYOTE!

Msomaji mpendwa, ikiwa Mungu Roho Mtakatifu amenena nawe, ikwa umejielewa kuwa mwenye dhambi mbele za macho ya Mungu anayestahili jehanum, sasa, nakusihi ili usimgeuzie Bwana Yesu Kristo mgogo wako, kwa sababu , "hakuna wokovo katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadanmu litupaswalo sisi kuokolewa kwalo." **(Matendo ya Mitume 4:12)**

Ikiwa utachangua kukataa njia ya Mungu ya pekee ya wokovu, sasa utakuwa na hakika kabisa ya kwamba unaenda Jehanum. "Sisi je! tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii." **(Waebrania 2:3)**

"Amwaminiye yeye (Yesu) hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu." **(Yohana 3:18)**

Lakini shukuru Mungu, ikiwa utatupu dhambi zako na kwa imani, umgeukie, na umtumaini Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana wako, unaweza kuwa na hakika kabisa ya kwamba unaenda Mbinguni!

"Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu." **(1 Yohana 5:13)**

"SASA basi, hakuna hukumu ya adhabu juu ya walio katika Kristo Yesu." **(Warumi 8:1)**

Mungu na akupe neema ya kuamini Neno lake la thamani kubwa na umulize akuokoe kutoka kwa dhambi zako leo.

Swahili

# Je, una hakika kabisa ya kwamba hutakaa JEHANUM milele?

# Je, una hakika kabisa ya kwamba hutakaa **JEHANUM** milele?

Habari njema kutoka kwa Neno la Mungu (Biblia) ni ya kwamba wanaume, wanawake, wavulana na wasichana WANAWEZA kuwa hakika kabisa ya kwamba hawatakaa JEHANUM milele!

Tafadhali chukua muda wakati muda uko, usome kijikartasi hiki and uwe hakika, leo utakaa wapi milele. Kama vila nchi iko vivyo hivyo Mbingu na Jehanum zimo, na nikatika mojapo ya hizi utakaa milele.

“Kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa, hukumu.” **(Waebrania 9:27)**

Unaweza kuuliza ni kwanini lazima hukumu iwepo. Jibu ni rahasi: kwa sababu Mungu ni mwema sana, ni lazima ahukumu dhambi. Ikiwa wale waliovunja sheria zake hawatahukumiwa, basi Mungu hatakuwa mwema.

Mungu ni Mtakatifu, Mwenye haki na Wakweli; ambaye tumeambiwa “kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka.” **(Yakobo 1:17)** Mungu hatageuza sheria zake kwa sababu ya yeyote yule, “kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti.” **(Warumi 6:23)** “Muhukumu ulimwengu wote asitende haki?” **(Mwanzo 18:25)**

Dhambi ni lazima ihukumiwe. Hata ikiwa ni mtu mmoja ataruhusiwa kuingia mbinguni kabla ya dhambi zake kuhukumiwa, basi Mungu atakuwa mwongo. “Mungu aonekane kuwa amini na kila mtu mwongo.” **(Warumi 3:4)**

Mungu amesema wasi katika Neno lake:sisi zote ni wenye dhambi, tumezaliwa katika dhambi kwa sababu ya uasi wa wazazi wetu wa kwanza, Adamu na Hawa. Neno la Munga tena lasema wasi ya kwamba sisi niwenye dhambi ambao wamekufa kiroho, na hatuwezi, kwa juhudi zetu wenyewe kujiokoa ama kujifanya wenye haki machoni pa Mungu.

“Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.” **(Warumi 3:23)** “Matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi.” **(Isaya 64:6)**

Kwa hiyo tunaona kutoka kwa neno la Mungu ya kwamba sisi ni wenye dhambi na ya kwamba Mungu ni lazima ahukumu dhambi.

“Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa hakiba kwa moto, kwa Neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.” **(2 Petro 3:7)**

“Bwana alikuja na watakatifu wake maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake.” **(Yuda 14 na 15)**

Namshukuru Mungu kwa sababu hakutuambia maneno haya tu! Msomsji mpendwa kuna tumaini, kuna njia ambayo kwayo twaweza kupatanishwa na Mungu Mtakatifu anaye chukia dhambi!

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” **(Yohana 3:16)**

Ni uzuri kiasi gani, ni neema kiasi gani! Mungu alimpeana Mwanawe, Yesu Kristo; “Neno (wa milele) alifanyika mwili, akakaa kwetu!” “Alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea” (Luka 19:10) “Ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi.” **(Wakolosai 1:14)**

Yesu Kristo, alilipa thamana mara moja tu wakati alipojitoa mwenyewe kwa ajili yetu, “Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akauhishwa.” **(1 Petro 3:18)**